# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 2

# KISWAHILI PAPER 3 ANSWER

## SEHEMU A (Alama 20 )

### USHAIRI : LAZIMA

1. (a) - Ukaraguni - Vina vya ndani na nje vinatofautiana.

- Tarbaia - Mishororo minne katika kila ubeti. (Hoja2xl=2)

(b) - Anatoa mwito kwa wanajamii waache kuendeleza ufisadi ambao una maovu tele. Anawahimiza wazingatie maadili ya jamii. (Hoja 1x3=3)

(c) - Udamisi umetumiwa katika ubeti wa tatu kukejeli wala hongo – wakiitisha hongo wapewe kikombe cha chai. (Hoja 1 x 2 = 2)

(d) - Suala rejelewa hongo ni kizingiti katika utoaji wa huduma za kimsingi katika jamii. (Hoja 1 x 2 = 2)

(e) - Kuboronga/kufinyanga sarufi - parapanda tunapinga badala ya tunapiga

parapanda - kuwe na urari wa vina.

Inkisari - mejaa badala ya yamejaa - kuwe na utoshelezo wa mizani katika mishororo.

Utohozi - kupasi watapasi - kuonyesha udhaifu wa lugha fasaha na ukengeushi.

Tabdila - masikini badala ya maskini - kuonyesha ukamilifu wa matamshi ya silabi. (Hoja 2 x 1 = 2 - lazima atoe mifano na kusanifisha)

(f) _____________

Nchi isipokuwa na ulaji rushwa/mlungula huwa na ustawi. Wakulima watafurahia mapato yao. Tusitumie hila bali walipwe kwa wakati ufaao. Maovu yamekithiri au yamezidi, heri tuyakomeshe. (Hoja zozote 3x1=3)

_____________

Barabara za orofa kama ya Thika zitajengwa. Usafiri utaimarishwa na kuinua uchumi. Wajenzi wakiwajibika, watawaridhisha Wakenya. Uovu umezidi, heri tuukomeshe. (Hoja4xl=4)

(g) - Toni ya chuki - Kadhongo kuwa na uvundo.

- Toni ya masikitiko/huzuni – matokeo ya hongo kuwa umaskini na huzuni. (Hoja 1 x1=1 )

(h) - Wapokeao hongo hutokana na kushawishika/majaribu kwa kuwa huletewa/hupokezwa. (Hoja 1x2 = 2)

## SEHEMU B (Alama 20 )

### RIWAYA K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea. Jibu swali la 2 au la 3.

2. (a) Msemaji ni Amani. Akimwambia Madhubuti wakiwa kwenye kibanda cha Amani.

Amani na Madhubuti walikuwa wanaongea kuhusu vitabu ambavyo wamesoma,vinanvyopendekeza mabadiliko katika jamii.Madhubuti anajutia vitendo viovu vya babake.
(b) (i) Mbinu za mapinduzi:
i) Mzee Matuko Weye kupanda jukwaani na kumwambia Mtemi Nasaba Bora kuhusu uongozi wake bila uoga.

ii) Madhubuti kumwandikia baba yake barua ya uasi na kukataa kazi aliyokuwa amepangiwa.

iii) Kulipa kisasi: Gaddafi anapanga kumpiga risasi Mtemi Nasaba Bora.

iv) Kusoma vitabu kuhusu mapinduzi k.v wretched of Earth,season of Migration to the North.

v) Kushirikiana/umoja:Amani na Madhubuti wanaungana kupindua uongozi wa Mtemi Nasaba Bora. Zozote (4x2=8)

3. - Taasubi ya kiume –Mtemi Nasaba Bora na nduguye mwalimu Majisifu wanawakandamiza wake zao

- Ufisadi uliokithiri - Mtemi kutumia cheo chake kumnyakua na kupokonya watu ardhiyao.
- Ufuska/uasherati - Mtemi Nasaba Bora kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Lowela ilhali ana mke Bi. Zuhura.

- Uanaharamu kukithiri - kuzaliwa kwa kitoto Uhuru kwa njia haramu kasha kinatelekezwa.

- Utawala wa kiimla — baadhi ya viongozi kama Mtemi Nasaba Bora kutawala kimabavu bila kushirikisha raia.

- Mapinduzi ya watawala hasi - raia wa Tomoko wanaongozwa na Amani kujikomboa.

- Ukoloni mambo leo - uendelezaji wa sera za utawala wa wakoloni wakonge. Mfano kurithi na kuisha katika kasri kwa Mtemi Nasaba Bora. Uasi wa vijana - vijana waliokengeuka na kuzinduka wanawaasi wazazi wao. Mfano: Madhubuti kumwasi babake.

- Uendelezaji wa harakati za ukombozi - wahanga wa ukombozi kama Amani na Imani wanavyokuiga kanda kufani - kasha juhudi zao. Kuvunjika kwa uchumba — Majinuni anavyokataliwa na Michelle; Ben Bella kumkataa Mashaka n.k.

- Mizozo katika ndoa - kuna mizozo katika ndoa za Mtemi Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu.

- Utapeli - Mwalimu Majisifu anaiba mswada wa Amani. (Hoja 10x2 = 20)

## SEHEMU C (Alama 20 )

### TAMTHILIA Timothy Arege:Mstahiki Meya Jibu swali la 4 au la 5.

4. (a) Haya ni maneno ya diwani II. Ni alasiri katika ofisi ya Meya, madiwani wameketi wakimsuburi Meya. Diwani II akiwaambia Diwani I na III kuhusu

jukumu lao la kumfaaa Meya.

(b) Dhana ya kufaa na kijifaa.

______

i) Diwani wa I na Diwani II wanamfaa Meya kwa kumuunga mkono katika uongozi wake

ii) Meya anawafaa madiwani kwa kuwaongezea mshahara na marupurupu.

iii) Kuwepo kwa mameya kunamfaa Dida, ataendelea kuwafanyia kazi.

iv) Bili anamfaa Meya kwa kumshauri kuhusu ufisadi k.m kisa cha mwanakandarasi na uuzaji wa fimbo.

v) Meya anamfaa Bili kwa kuipeleka familia yake kustarehe.

vi) Siki anawafaa wagonjwa kwa kuwapa matumaini.

vii) Siki anawafaa wafanyikazi kwa kuwatetea kwa Meya.

viii) Viongozi wa wafanyikazi (Tatu, Beka na Medi) wanawafaa wafanyikazi kwa kuwatetea.

ix)Meya anamfaa mhubiri kwa kumpa mafuta ya gari/kumpa shilingi laki moja kila mwezi.

x) Diwani III anawafaa wanacheneo kwa kuwatetea dhidi ya utawala dhalimu wa Meya Sosi. (yoyote 8x1=8)

i) Meya anatumia mali ya cheneo kuwapeleka watoto wake kusomea ng'ambo na mkewe kujifungulia ng'ambo.

ii) Meya ananyakua vipande vya ardhi.

iii) Bili anamshauri Meya ili kujinufaisha kutoka kwa Meya k.m kisa cha mwanakandarasi na kuuza fimbo, kustarehe n.k

iv) Diwani I na Diwani II wanajipendekeza kwa Meya ili kujinufaisha kwa mshahara na marupurupu.

v) Dida anafanya kazi kwa Mameya ili apate riziki.

vi) Meya anatoa ahadi za uongo k.m Kuwa dawa ziko njiani ili aendelee kuwa uongozini.

vii) Mhubiri anaenda kumwombea Meya ili ajiinufaishe kwa sadaka.

viii) Meya anapendelea wageni wafike cheneo ili anufaike na pia cheneo inufaike kimaendeleo. (8x1 =8) 5

5.

i) Siki anafanya juhudiya kumtembelea Meya ili kuwasilisha hali mbaya ya Wanacheneo

ii) Siki anafanya juhudiya kumtembelea Diwani III ili amtume awasilishe matatizo ya wanacheneo kwa Meya.

iii) Diwani wa III anakataa kukubaliana na maoni ya Meya na madiwani wenzake wa I na iv) wa II kuhusu nyongeza ya mishahara na marupurupu.

v) Wafanykazi wanagoma kudai mishahara mizuri.
vi) Tatu, Beka na Medi wanaenda kumwona Meya kulalamikia mazingira magumu ya kazi. (5x2=10)

i) Baraza la Cheneo halina dawa.

ii) Wafanyakazi wa Cheneo wanagoma kwa sababu ya mishahara duni

iii) Mji wa Cheneo una uvundo kwa sababu takataka haikuzolewa.

iv) Wafanyakazi wa Cheneo hawana vifaa vya kazi k.v glavu.

v) Viongozi kama Meya wananyakua vipande vya ardhi.

vi) Viongozi kama Meya wanashiriki katika mauzo ya fimbo ambayo ni nembo ya uongozi.

vii) Meya anawaongoza madiwani na kuwabagua wafanyikazi wengine.(Ubaguzi).(zozote 5x2=10

## SEHEMU D (Alama 20 )

**; HADITHI FUPI K. W. Walibora na S. A. Mohamed (Wah.): Damu Nyeusi na Hadithi Nynyingine. Kikaza (Robert Oduor) Jibu swali la 6 au la 7. 6**

6. (a)- ____________________

- Anamwambia Bw. Mwatela,

- Mahali ni nyumbani kwa Bw. Mwatela.

- Kananda amemwuliza Bw. Mwatela lini angemwoa baadaya kumtinga. (Hoja4xl=4)

(b)- ____________________________________________

- Anamwomba Kananda kuhifadhi siri kuhusu hali yake ya uja uzito.

- Anamweleza amhadae Mama Sami kuwa mimba ilikuwa ya rafiki yake mmoja kule kwao,si ya Bw. Mwatela.

- Anamhadaa kwamba angemwoa baada ya kujifungua.

- Mama Sami anashawishika kwa uongo wa Kananda na kuahidi kumsaidia atakapojifungua. (Hoja4xl=4)

(c)- ________________________________________________________________________

- Tatizo la uzazi -Bwana na Bi. Mwatela wana mtoto mmoja tu na anapofariki wanafadhaika.Inabidi wamtwae Mwakitawa.

- Kukidhi mahitajiya watoto/malezi

- inabidi wazazi wake Kananda wamwajirishe ili wapate mahitaji.

- Taasubi ya kiume - Bw. Mwatela anaendeleza ubabedume kwa ukatili dhidi ya mkewe Mama Sami.

- Matatizo ya ukewenza - Bw. Mwatela anahofia mkewe kufahamu kuwa yeye ndiye aliye sababisha uja uzito wa Mwatela. Anatisha kumwua Kananda iwapo angefichua siri.

- Jukumu la malezi ni la wazazi - Bw. Mwatela anajitolea kumtunza Mwakitawa kwa gharama zote.

- Uanaharamu kutokea na kuathiri maisha ya ndoa - Mwakitawa kuwa chanzo cha mtafaruku bainaya Mwatela na mkewe. (Hoja 5 x 2 = 10)

7. ___________________________

**a) <u>Mke wangu.</u>**

i) Msimulizi anamtaka mwanamke ambaye angemdhibiti.

ii) Mume anachaguliwa mke; mke hana hiari.

iii) Mavazi ya mwanamke yawe yanayokubaliwa.

iv) Mwanamke hastahili kutembea usiku.

b) ______________________

i) Peter anamtumia Christine kimapenzi na kumuacha.

ii) Peter huwatumia wasichana na kuwaacha, anavyoona Deogracius.

iii) Peter anapoambiwa kuhusu uavyaji wa mimba na Christine, anapuuza tu.

c) _______

i) Duni alikuwa akimpiga Jamila.

ii) Duni alikuwa akilewa na kumwacha Jamila katika upweke.

iii) Duni alimuudhi Jamila kwa kelele na matusi.

d) ______________

i) Chris Masazu anampachika mimba Sela.
ii) Sela anapomwambia kuhusu mimba, Chris anapuuza tu; anamwambia "Yajapo yapokee

iii) Sela analazimika kukoma shule ili ajifungue mtoto.

iv) Babake Sela, Mzee Butali, anamlaumu mamake Sela kwa kosa la Sela kupata mimba.

e)_

i) Kananda anapachikwa mimba na Mwatela.

ii) Baadaya kujifungua Kananda ananyang'anywa mtoto wake.

iii) Kananda anachukuliwa na dereva wa malori kutoka Kongo.

iv) Kananda anataabika kurudi nyumbani.

v) Mwatela anamdanganya Mwakitawa, kisha Mwakitawa anamrushia jiwe Kananda na kumuumiza vibaya. Hadithi 5x4 =20 Kutaja hadithi 1 Dhuluma 3 kwa kila hadithi 3 x 1=3

## SEHEMU E (Alama 20 )

### FASIHI SIMULIZI: Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

9. (a) Kipera cha maapizo. (alama 1)

(b) Nafsineni ni mama mkwe kwa mke wa mwanawe. (alama 1)

(c) __________________

i) Hutolewa kwa watu wanaoenda kinyume na matarajio ya jamii zao.

ii) Katika baadhi ya jamii za kiafrika, maapizo hutolewa kabla ya ulaji wa viapo.

iii) Maapizo yanaweza kutolewa moja kwa moja na aliyeathirika.

iv) Kidini, Mungu, miungu au mizimu huweza kutoa maapizo kuhusu yanayomkabili mhusika Fulani. Aidha, maapizo ya kidini yanaweza kutolewa kama laana.

v) Huaminiwa kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, kwa hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema

. vi) Maapizo hutumia lugha fasaha (Ulumbi).

vii) Hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidiya maovu. (5x2=10)

d) ________________________________

i) Hutumiwa kama nyenzo ya kuwaonya wanajamii dhidi ya matendo hasi.

ii) Hutambulisha jamii- Kila jamii ina namna yake ya kuapiza na mitindo tofauti ya kutoa maapizo.

iii) Hukuza umoja katika jamii- Kuwapo kwa kaida na miiko sawa, huwafanya iv) watu kujihisi kuwa kitu kimoja..

v) Huadilisha - wanajamii hujifunza kutenda mema ili kuepuka laana. (4x1=4)

e) i) Husaidia kurekodi fasihi simulizi hivyo kuirithisha kwa vizazi vipya.

ii) Husaidia kuibua sifa za kimsingi za vipera vya fasihi simulizi.

iii) Husaidia kulinganisha fasihi za jamii mbalimbali na kuonyesha tofauti zake.

iv) Matokeo ya utafiti wa nyanjani husaidia kuziba mapengo yaliyopo ya utafiti.

v) Ukusanyaji na uhifadhi huendeleza fasihi simulizi kwa vizazi vijavyo.

vi) Ni muhimu kutafiti kuhusu fasihi simulizi ili kusahihisha mawazo potofu kuhusu baadhi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi. (Hoja zozote 4x1=4)